TANGAZO LA SERIKALI NA. 266 la tarehe 12/4/2024

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA YA WILAYA), (SURA YA 287)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 153 (1) (b))*

SHERIA NDOGO YA UDHIBITI NA USIMAMIZI WA MIFUGO YA HALMASHAURI YA MANISPAA YA SHINYANGA YA MWAKA 2024

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Udhibiti na Usimamizi wa Mifugo ya Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga ya Mwaka 2024.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote lililopo chini ya Mamlaka ya Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga;

"kibali" maana yake ni idhini ya maandishi inayotolewa na Halmashauri kwa ajili ya kufanya shughuli iliyokusudiwa chini ya Sheria Ndogo hii;

"maeneo ya malisho" ni pamoja na sehemu zote ambazo Halmashauri itatenga kuwa eneo la malisho;

"mfugaji" maana yake ni mtu yeyote anayejishughulisha na ufugaji wa mifugo katika eneo la Halmashauri;

"mfugo" maana yake ni ng'ombe, mbuzi, kondoo, kuku, na wanyama wengine wafugwao;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga au Afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"Wakala" maana yake ni mtu binafsi, kikundi, taasisi, shirika au kampuni iliyoteuliwa kwa ajili ya kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii.

Wajibu wa Halmashauri

4. Halmashauri itakuwa na wajibu wa kufanya mambo yafuatayo:

(a) kuandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi;
(b) kutenga maeneo maalumu kwa ajili ya shughuli ya ufugaji kwa mujibu wa Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi;
(c) kujenga majosho ya mifugo kwa kushirikiana na wananchi;
(d) kutoa elimu ya ufugaji bora kwa jamii ili kuongeza tija;
(e) kufanya sensa ya mifugo, kuweka alama na kutoa kadi za mifugo;
(f) kutoa chanjo kwa kushirikiana na wafugaji ili kudhibiti magonjwa ya mifugo yasiyoambukiza na yanayoambukiza binadamu; na
(g) kudhibiti uzururaji holela wa mifugo na wanyama katika Halmashauri kwa mujibu wa Sheria.

Wajibu wa mfugaji

5. Kila mfugaji chini ya Sheria Ndogo hii atahakikisha kuwa:

(a) anaogesha mifugo yake katika majosho ili kudhibiti magonjwa ya wanyama kama atakavyoelekezwa na Halmashauri;
(b) anachangia gharama za ukarabati wa majosho kama sehemu ya mchango wake, pale itakapobidi kufanya hivyo, na kwa gharama itakayopendekezwa na Halmashauri;

(c) anafuga na kulisha mifugo yake katika maeneo yaliyoteuliwa na Halmashauri;
(d) anachangia gharama za uboreshaji wa maeneo ya malisho yaliyoainishwa na Halmashauri;
(e) anapeleka mifugo yake katika vituo vya chanjo kama itakavyoamriwa na Halmashauri na atalipia chanjo hiyo kama atatakiwa kufanya hivyo kwa mujibu wa viwango vitakavyoainishwa na Mamlaka husika;
(f) mifugo yake inawekwa alama maalumu zinazotolewa kwa mujibu wa Sheria na miongozo bila kuharibu zao la ngozi;
(g) anafuga idadi ya mifugo kama itakavyoamriwa na Halmashauri;
(h) hatakaribisha wafugaji wengine bila kibali cha Halmashauri;
(i) anaipaa mifugo yake malisho au chakula na maji ya kutosha kwa kuzingatia kanuni bora za ufugaji;
(j) anapitisha mifugo yake katika njia maalumu zilizopangwa na kuainishwa na Halmashauri;
(k) ana kibali cha kusafirisha mifugo na mazao yake;
(l) kabla ya kuingiza mifugo katika Halmashauri anaomba kibali cha maandishi cha kukubaliwa kuingiza mifugo hiyo ndani ya Halmashauri;
(m) anafuga kwa kuzingatia mipango ya matumizi bora ya ardhi;
(n) ana kadi ya mifugo itakayoonesha idadi na aina ya mifugo aliyonayo;
(o) anahudhuria mafunzo ya ufugaji kama atakavyo hitajika na Halmashauri;
(p) anauza mifugo yake katika masoko na minada iliyoidhinishwa au eneo lingine kwa taarifa maalum; na
(q) anapakia mifugo yake katika maeneo ya Serikali

au ya mtu binafsi yaliyoidhinishwa na Halmashauri kwa kulipia gharama zitakazoainishwa kwa kipindi husika.

Kibali cha ufugaji

6.-(1) Mtu anayetaka kufuga mifugo atalazimika kupata kibali cha kufuga kutoka kwa Halmashauri kama kilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hii.

(2) Bila kuathiri kanuni ndogo ya (1), mtu yeyote atakayekiuka taratibu za ufugaji kulingana na Sheria Ndogo hii kibali chake kitafutwa na atalazimika kuhamisha mifugo yake yote.

Masharti kwa mfugaji

7. Mfugaji hataruhusiwa-

(a) kuchunga, kulisha au kunywesha maji mifugo katika maeneo ambayo hayajatengwa kwa shughuli hiyo;
(b) kuwatumia watoto hasa wenye umri wa kwenda shule kuchunga au kuhudumia mifugo;
(c) kusafirisha mifugo kwa kuiswaga barabarani;
(d) kusafirisha au kuhamisha mifugo kutoka eneo moja hadi lingine bila kibali kutoka Halmashauri;
(e) kuingiza mifugo katika eneo la Halmashauri bila kibali kinachotolewa na Afisa Kilimo, Mifugo na Uvuvi wa Halmashauri;
(f) kuuza au kununua mifugo katika maeneo ambayo si mnada, masoko au magulio ya mifugo yaliyoidhinishwa bila kibali maalumu cha Halmashauri;
(g) kulisha mifugo kwenye maeneo ya kilimo au wakulima kuruhusu mifugo kwenye maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya kilimo;
(h) kupitisha mifugo katika maeneo ambayo hayajaidhinishwa na Halmashauri kupitisha mifugo;

(i) kufuga mifugo mingi katika eneo dogo ndani ya Halmashauri; au

(j) kununua, kuuza au kufanya biashara ya kubadilishana aina yoyote ya mfugo katika eneo la Halmashauri bila kibali maalumu isipokuwa kwenye masoko, minada au magulio yaliyotengwa kwa ajili ya shughuli hiyo na Halmashauri.

Kibali cha kusafirisha mifugo na mazao au chakula chake

8.-(1) Mtu anayetaka kusafirisha mifugo na mazao au chakula ch mifugo kutoka au kuingia katika eneo la Halmashauri atatakiwa kupata kibali maalumu kama kilivyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hii.

(2) Halmashauri itatoa kibali cha kusafirisha mifugo na mazao au chakula cha mifugo kwa kuweka utaratibu ikiwa ni pamoja na:

(a) mfugaji kutoa uthibitisho wa umiliki wa mfugo au uthibitisho kutoka kwa Afisa Mwidhiniwa; na

(b) kukagua kibali cha kusafirisha mfugo na mazao au chakula cha mifugo.

(3) Afisa Mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa kukamata na kutoza faini kwa ajili ya mfugo au mifugo na mazao au chakula cha mifugo kinachosafirishwa kinyume na Sheria Ndogo hii.

Taratibu za ufugaji

9. Mfugaji atatakiwa kuzingatia masharti ya kufuga kama yalivyoainishwa katika Sheria Ndogo hii na sheria nyingine za nchi.

Kuchinja mfugo

10. Mtu anayetaka kuchinja mfugo wake atatakiwa kupeleka mfugo huo machinjioni au ikiwa ni mahali pasipo machinjio kwa kibali maalumu cha Afisa Mwidhiniwa.

Kudhibiti mifugo inayozurura ovyo

11.-(1) Halmashauri itakamata mifugo itakayoonekana inazurura ovyo katika eneo la Halmashauri na mmiliki atatakiwa kulipia faini kwa kiasi kama

kilivyoainishwa katika Jedwali la Tatu la Sheria Ndogo hii kama gharama za kuhifadhi mifugo hiyo.

(2) Endapo mfugo uliokamatwa hautachukuliwa na mmiliki ndani ya kipindi cha siku saba tangu kukamatwa, Halmashauri itakuwa na haki ya kuuza mnada mfugo huo baada ya kupata idhini ya Mahakama, na fedha zitakazopatikana zitarejeshwa kwa mmliki wa mfugo huo baada ya kutoa faini inayodaiwa, gharama za kuhifadhi mfugo, gharama ya Mahakama na gharama ya mnada.

(3) Bila kuathiri kanuni ndogo ya (2), Halmashauri kabla ya kuuza mfugo huo kwa mnada itamjulisha mmiliki na umma kuhusu kusudio hilo.

(4) Endapo kutatokea kufa kwa mifugo au mfugo kutokana na sababu yoyote, Halmashauri haitawajibika na ulipaji wa gharama zozote isipokuwa kama vifo hivyo vitakuwa vimesababishwa kwa uzembe wa watumishi wa Halmashauri.

Ukaguzi wa mifugo na bidhaa za mifugo

12. (1) Afisa Mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa kukataa aina yoyote ya mifugo au bidhaa kuingia au kuuzwa ndani ya eneo la Halmashauri, iwapo mifugo hiyo au bidhaa hizo zinaweza kuhatarisha afya au usalama wa mifugo mingine au watumiaji.

(2) Afisa Mwidhiniwa anaweza kuingia katika nyumba au jengo lolote kuanzia saa kumi na mbili asubuhi hadi saa kumi na mbili jioni kwa lengo la utekelezaji wa Sheria Ndogo hii.

Taratibu za biashara ya mifugo na mazao yake

13.-(1) Mfanyabiashara kabla ya kuanza biashara ya mifugo na mazao ya mifugo atatakiwa kuwa na leseni na vibali kutoka Mamlaka husika vinavyohusu kuuza na kununua mifugo na mazao ya mifugo na atatakiwa kuwasilisha vibali vyake Halmashauri kwa ajili ya uhakiki.

(2) Mfanyabiashara wa mifugo inayopelekwa au kutoka mnadani au machinjioni atatakiwa kuwa na kibali maalumu kutoka Halmashauri.

(3) Mfanyabiashara atakayesafirisha mifugo kutoka nje ya Halmashauri atatakiwa kuwa na kibali kutoka Halmashauri ambayo mifugo hiyo inatoka.

(4) Bila kuathiri masharti yaliyowekwa katika kanuni ndogo ya (2) na (3), mfanyabiashara wa mifugo atatakiwa kusafirisha mifugo katika vyombo vya usafiri vinavyokubalika kwa mujibu wa sheria.

(5) Mifugo yote itauzwa au kununuliwa katika minada na masoko yanayotambulika kwa mujibu wa sheria.

(6) Minada yote ya mifugo au magulio ya mifugo yatafanyika kwa kibali maalumu cha Halmashauri na kwenye maeneo yaliyoruhusiwa.

Makosa

14. Mfugaji anatenda kosa iwapo:
- (a) atashindwa au kukataa kuogesha au kuchanja mfugo au mifugo yake ili kuzuia magonjwa;
- (b) atalisha mfugo au mifugo kwenye maeneo yasiyoruhusiwa;
- (c) ataruhusu mfugo au mifugo yake kuzurura ovyo;
- (d) atamshawishi mtu au kundi la watu kuingiza mifugo ndani ya Halmashauri bila kuzingatia sheria, kanuni na taratibu;
- (e) hatakuwa na kibali cha ufugaji;
- (f) atashindwa au atazembea kutoa taarifa juu ya uwepo wa dalili za ugonjwa au kifo cha ghafla cha mfugo katika banda lake;
- (g) atashindwa kutoa ushirikiano wa uwekaji wa alama kwa mfugo au mifugo yake;
- (h) atamruhusu mtu yeyote ambaye hana utaalamu wa vyakula vya mifugo kujihusisha na utengenezaji wa vyakula vya mifugo; au
- (i) atamzuia Afisa Mwidhiniwa kutekeleza majukumu yake.

Adhabu

15. Mtu atakayepatikana na hatia kwa kutenda kosa

chini ya Sheria Ndogo hii atawajibika kulipa faini ya kiasi kisichopungua Shilingi elfu hamsini na kisichozidi Shilingi laki tatu au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili jela au vyote.

Kufifilisha kosa

16. Mkurugenzi anaweza kumtoza faini mtu yeyote aliyetenda kosa chini ya Sheria Ndogo hii, kiasi kisichozidi shilingi elfu hamsini iwapo mkosaji atakiri kosa kwa hiari na kuwa tayari kujaza fomu maalumu iliyoambatanishwa kwenye Jedwali la Nne la Sheria Ndogo hii.

## JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 6 (1))*

### KIBALI CHA KUFUGA MFUGO

Jina la Mfugaji: …………………………………………………
Anuani: …………………………………………………………
Kata: …………………………………… Mtaa …………………
Namba Nyumba:…………………………………… Namba Kitalu:……………
Ameruhusiwa kufuga Mifugo ifuatayo katika eneo la…………...

| Na | Aina ya Mfugo | Koo | Idadi ya Mifugo | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Jike | Dume | |
| 1 | Ng'ombe | | | | |
| 2 | Mbuzi | | | | |
| 3 | Kondoo | | | | |
| 4 | Nguruwe | | | | |
| 5 | Ngamia | | | | |
| 6 | Punda | | | | |
| 7 | Paka | | | | |
| 8 | Farasi | | | | |
| 9 | Sungura | | | | |
| 10 | Mbwa | | | | |
| 11 | Kuku au Bata | | | | |
| 12 | Wanyama | | | | |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | wengine | | | | |

Kibali hiki kimetolewa kwa Ndugu……………………………………kwa muda wa miezi kumi na mbili kwa Mfugo au mifugo kuanzia tarehe……………...hadi tarehe…………...

Kimetolewa na:
Jina la Afisa Mwidhiniwa…………………………………..Saini……....................…
Wadhifa:……………………………………………………......................………..
Tarehe:…………………..............................................................................................
Muhuri:………………………………………….....................................................

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 8)*

KIBALI CHA KUSAFIRISHA MIFUGO NA MAZAO AU VYAKULA VYA MIFUGO

Kibali Na: …..................................................................
Jina: …..........................................................................
Anuani: ….....................................................................

1. Ameruhusiwa kusafirisha Mifugo ifuatayo kutoka ………………kupitia njia za……………………..hadi…………..…..

| Namba | Aina ya Mfugo | Idadi ya Mifugo |
|---|---|---|
| 1. | Ng’ombe | |
| 2. | Mbuzi | |
| 3. | Kondoo | |
| 4. | Nguruwe | |
| 5. | Ngamia | |
| 6. | Punda | |
| 7. | Paka | |
| 8. | Farasi | |
| 9. | Sungura | |
| 10. | Mbwa | |
| 11. | Kuku au Bata | |
| 12. | Mifugo wengine | |

2. Ameruhusiwa kusafirisha Chakula cha mifugo aina ya
…........................................................ Uzito: ….............................................
Kutoka: …......................................................... kwenda:
…......................................................
Kupitia:
…...............................................................................................................................
Njia ya usafirishaji: …............................................
Namba ya usajili wa Gari: …....................
Kibali hiki kimetolewa tarehe: …../......... 20 ...... na kitatumika hadi tarehe: …..../....... 20 ……

TAARIFA YA CHANJO AU MATIBABU:
...…...................................................................……………………………………………….
...…...................................................................……………………………………………….

Hali ya wanyama wakati wa usafirishaji:
…..........................................................................................
…..........................................................................................................................................

Kibali hiki kimetolewa hapa:
Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga Tarehe: ........../.............. 20.........
Jina la Afisa Mwidhiniwa: ............................................................................
Saini: ….......................................................................
Wadhifa: ..…...............................................................

Mhuri wa Ofisi…………………………..

## JEDWALI LA TATU

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 11)*

VIWANGO VYA MALIPO YA KUHIFADHI MIFUGO ILIYOKAMATWA NA HALMASHAURI KWA KILA MFUGO

| Na | Jina la Mfugo | Kiasi | Siku |
|---|---|---|---|
| 1. | Ng`ombe | 2500 | 1 |
| 2. | Mbuzi au Kondoo | 1500 | 1 |

*Tangazo La Serikali Na. 266 (Linaendelea)*

| | | | |
|---|---|---|---|
| 3. | Nguruwe | 1500 | 1 |
| 4. | Punda au Farasi au Ngamia | 2500 | 1 |
| 5. | Mbwa au Paka | 1000 | 1 |

JEDWALI LA NNE

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 16)*

FOMU YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA

Mimi ……………………………………………………… nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya …………………………………………. ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga, kwamba mnamo tarehe …… ya Mwezi ………. Mwaka ……….…… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kanuni ya …… ya Sheria Ndogo ya Udhibiti na Usimamizi wa Mifugo ya Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga ya Mwaka 2024.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga, Niko tayari kulipa kiasi cha faini ya shilingi .......................................... badala ya kushtakiwa Mahakamani.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA MIMI MWENYEWE KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU
Leo tarehe…………. ya Mwezi…………..… Mwaka …………….
Jina……………………………….. Saini……………………….......
MBELE YANGU:
Jina:…………………………………..…………………......…
Saini………………………….…………………………..………
Wadhifa……………………………………………....…………
Tarehe………………………………………………………....

Lakiri ya Halmashauri ya wilaya ya Shinyanga imegongwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufutia azimio lililopitishwa katika Mkutano uliofanyika Tarehe 23-24/3/2023 na kushuhudiwa Lakari hiyo ikigongwa mbele ya;

MWL ALEXIUS REVOCATUS KAGUNZE
*Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga*

MH. ELIAS RAMADHANI MASUMBUKO
*Mstahiki Meya wa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga*

NAKUBALI

L.S

Dodoma,
30 Januari, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA
*Waziri wa Nchi- Ofisi ya Rais (Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa)*